Sheria za udereva

Driving Laws - Swahili

Karatasi hii inaelezea baadhi ya vigezo vya msingi ili kupata leseni ya udereva katika Australia ya Magharibi na inaelezea baadhi ya makosa ya barabarani. Sio ufafanuzi wa kina wa sheria ya udereva na hivyo utahitaji kutafuta ushauri wa kisheria endapo utapatwa na tuhuma za barabarani.

Udhibitisho wa madereva

Katika Australia, ni kosa kuendesha:

- Bila ya kuwa na daraja sahihi la leseni ya udeleva kulingana na gari unaloliendesha
- Wakati unaendesha leseni yako imesitishwa, imefutwa au imeisha muda wake
- Wakati huna sifa za kupewa au kumiliki leseni ya udereva.

Kuna adhabu maalumu kwa kutenda kosa barabarani zinazo jumuisha (hefty)faini na ikibidi kufungwa jera.

Kabla ya kupewa leseni yako utalazimika kupatiwa ruhusa ya mafunzo kutoka idara ya usafiri. Hasa pale ufikiapo angalau miaka 16, unaweza sasa kufanya mtihani ili kupata ruhusa hiyo ya mafunzo.

Kuna masharti maalumu huwekwa wakati unatumia ruhusa ya mafunzo. Nikosa kusa kutofuata masharti hayo katika ruhusa ya mafunzo. Kwa mfano, hauta endesha pasipo kuwa na mtu mwenye utaalamu wa kutosha wa kuendesha angalau wa miaka mine.

Ili kupata leseni yako ya udereva lazima ufaulu majalibiao, vitendo, ukamilishe angalau masaa 25 ya uendeshaji chini ya uangalizi na ukamilishe majalibio ya kugundua hatari.

Utoaji leseni wa magari

Magari yote lazima yawe yamesajiliwa katika idara ya huduma za leseni za usafilishaji.

Nikosa kuendesha gari kubwa katika barabara yoyote ile iwapo gari hili halina leseni halali ya gari. Mtu yoyote atakaye endesha gari au atakaye ruhusu gari litumike katika barabara yoyote atakuwa anafanya makosa. Mahakama inaweza kukuagiza ulipe faini kubwa kwa kufanya kosa hilo.

Kuendesha wakati umelewa pombe au madawa ya kulevya

Mtu yeyote atakaye endesha gari akiwa amelewa pombe au madawa kwa kiasi cha kutoweza kulitawala gari hilo, atakuwa mkosaji kwa kuendesha akiwa hajiwezi. Kuendesha ukiwa hujiwezi ni vibaya na adhabu yake ni kali mno.

Sheria za ulevi wakati unaendesha zinaelekeza kiasi cha mwisho cha alkoholi ya pombe kutegemea na mambo kadhaa, ikijumuisha miaka mingapi umekuwa unamiliki leseni ya udeleva. Kwamfano mtu ambaye amekuwa akimiliki leseni kwa kipindi cha chini ya miaka miwili atakuwa na kikomo cha kiasi cha alikoholi katika damu kisichozidi 0.00% na mtu anaye miliki leseni kamili kikomo chake cha alkoholi katika damu itakuwa 0.05%.

Iwapo utasimamishwa na polisi na kutakiwa ufanye majaribio ya awali ya pumzi utapaswa kufanya hivyo. Iwapo utakataa kufanyiwa jaribio la awali la pumzi polisi anaweza tena kukutaka tena kufanya jaribio la pumzi. Kukataa kufanya jaribio la pumzi ni kosa.

Iwapo polisi wataamini unadalili ya kutumia madawa yaliyo pingwa marufuku, hapo wanaweza kukutaka kufanyiwa jaribio la udereva na kipimo cha damu au mkojo. Kushindwa kutimiza jaribio la udereva au

KANUSHO: Maelezo ya karatasi hii yanatoa mwongozo wa jumla tu na yasitumiwe badala ya ushauri wa kisheria. Kwa kiwango cha juu kinachoruhusiwa na sheria, CASE kwa wakimbizi Inc. inakanusha hasara yoyote ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja itakayompata msomaji ikihusiana na kutegemea au kuhusiana na maelekezo katika karatasi hii. Msomajai lazima apate ushauri wa kisherai maalumu kutokana na mazingira ya mtu mwenyewe binafsi.

kuruhusu kuchukuliwa kiasi cha mkojo au damu utakaochukuliwa kwa ajili ya upembuzi ni kosa. Iwapo ukikutwa unaendesha ukiwa umelewa madawa, adhabu ni kubwa, ikihusishwa kupoteza leseni yako ya kudereva, na viwango vya adhabu vitaongezeka iwapo utatuhumiwa kwa mara nyingine tena.

Udereva wa kizembe, hatari na kutokuwa makini

Undeshaji wa kizembe ni kosa na unamaanisha uendeshaji wa makusudi ambao kwa kawaida ni hatari kwa umma. Mwendo kasi wa ziada ni mfano wa udereva wa kizembe. Utapoteza leseni yako ya udereva iwapo utakutwa unaendesha kizembe na kuambatana na faini kubwa. Unaweza hata kufungwa na polisi wanaweza kutaifishwa na gari lako kwa siku 28.

Uendesha wa hatari ni tuhuma na una maanisha uendesha hatari kwa umma.
Iwapo utashitakiwa kwa uendeshaji wa hatari, utatakiwa kulipa faini kubwa. Iwapo utatuhumiwa kwa mara nyingine utapoteza leseni yako ya udereva na kifungo ni mbadala

Uendeshaji usio makini ni tuhuma na umaanisha uendeshaji usiokuwa na uangalifu na umakini iwapo utashitakiwa utatakiwa kulipa faini kubwa.

Katika makosa yote kiwango cha adhabu huongezeka kadri tuhuma inavyorudiwa na kifungo kinawezekana.

Wapi pa kupata msaada?

CASE kwa wakimbizi ni kituo cha jamii cha kisheria kisicho kuwa cha kiserikali, dini ambacho hutoa huduma za uhamiaji na kisheria kwa ujumla kwa jamii za Australia ya magharibi zenye mtawanyiko na tamaduni na lugha. CASE inaweza kukusaidia na hoja ulizonazo zihusuzo sheria za uendeshaji (udereva) katika Australia na huweza kusaidia endapo utakabiliwa na tuhuma za barabarani. Adhabu za tuhuma za barabarani zinaweza kuwa kubwa sana hivyo unapaswa kutafuta ushauri wa kisheria hasa iwapo itakuwa siyo tuhuma yako ya kwanza.

Huduma zote sio za malipo, ingawa misaada ya watu binafsi na mashirika inapokelewa kwa ukarimu. Michango yote ya zaidi ya AUD $2.00 haina vati.

Mawasiliano ya CASE kwa wakimbizi inc.ni haya yafuatayo :

145 Stirling Street, Perth
Western Australia 6000

Simu:(08) 92277311

Kinukushi: (08) 92277188

Email:admin@caseforrefugees.org.au

KANUSHO: Maelezo ya karatasi hii yanatoa mwongozo wa jumla tu na yasitumiwe badala ya ushauri wa kisheria. Kwa kiwango cha juu kinachoruhusiwa na sheria, CASE kwa wakimbizi Inc. inakanusha hasara yoyote ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja itakayompata msomaji ikihusiana na kutegemea au kuhusiana na maelekezo katika karatasi hii. Msomajai lazima apate ushauri wa kisherai maalumu kutokana na mazingira ya mtu mwenyewe binafsi.